

# UANDISHI WA KITABU KINACHOUZIKA

*Siku 25 za kuwa mwandishi aliyefanikiwa bila **stress***

DAUDI LUBELEJE

Chapa ya kwanza
Hatimiliki © 2022

Daudi Lubeleje
+255 764 771 298, daudipages@mailfence.com
Arusha, Tanzania

Sanifu kurasa & jalada:
DL Bookstore,
+255 787 163 013, authors@dlbookstore.com
Arusha, Tanzania

ISBN 978 9976 50010 3

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuhifadhi, kuchapisha kwa njia ya kielektroniki au mekaniki, kutoa vivuli, kurekodi au kubadili sehemu yeyote ya kitabu hiki kwa njia, namna na mfumo wowote bila idhini ya maandishi kutoka kwa mchapishaji.

**Siku 25 zitakuwa na nini?*

# YALIYOMO


Dibaji........................................................ vii

Utangulizi.................................................... ix

**Siku 1.** Tabia 5 zinazoleta mafanikio kwa mwandishi.................................................... 1

**Siku 2.** Fanyia kazi mambo haya manne (4) ufanikiwe zaidi............................................ 5

**Siku 3.** Unaupataje muda wa kuandika kitabu?.. 9

**Siku 4.** Kama unataka kutoa kitabu, fuata hatua hizi.............................................................. 13

**Siku 5.** Swali moja wanalouliza sana wanaotaka kutoa eBook................................................ 17

**Siku 6.** Sababu nne (4) ugumu wa kuandika kitabu uko wapi?.................................................. 21

**Siku 7.** Jinsi ya kuandika 'kuhusu kitabu' inayonasa wasomaji wasome kitabu chako............ 25

**Siku 8.** Hatua tano (5) za kuwatambua wasomaji wako walengwa.................................. 29

**Siku 9.** Sehemu tatu zinazounda uzinduzi wa kitabu.......................................................................... 33

**Siku 10.** Ufanye nini uzinduzi wa kitabu chako unapofeli?.............................................................. 41

**Siku 11.** Jinsi ya kujenga jukwaa lako kama mwandishi.................................................................. 45

**Siku 12.** Makosa 4 wanayofanya waandishi wanapotangaza vitabu vyao................................ 53

**Siku 13.** Njia nne (4) za kumsaidia mwandishi kuongeza baruapepe za wasomaji wake................. 57

**Siku 14.** Hizi ndizo sababu kitabu chako hakiuzi............................................................................ 61

**Siku 15.** Fanya mambo haya matatu (3) uuze sana kitabu chako............................................ 65

**Siku 16.** Mambo 3 ya kuzingatia kupata jina la kitabu linalouza sana.......................................... 69

**Siku 17.** Jalada la kitabu lina kazi moja tu.......... 73

**Siku 18**. Maswali matano (5) ya kujiuliza kabla ya kuamua jalada ulilonalo litumike kwenye kitabu............................................................... 77

**Siku 19.** Kwanini mwandishi afanye book cover makeover?.......................................................... 81

**Siku 20.** Njia 4 za kupata "reviews" za wasomaji wa kitabu chako................................................ 85

**Siku 21.** Mambo ya kuzingatia kabla ya kusoma kitabu................................................................ 89

**Siku 22.** Unajua kava la kitabu bora huzingatia kanuni 3? Soma hapa........................................ 93

**Siku 23**. Andaa mambo haya kwanza kabla ya kufikiria kupata jalada la kitabu.......................... 97

**Siku 24**. Kama mwandishi wa vitabu unataka kufanikiwa kwenye nini?.................................... 103

**Siku 25.** Kuandika kitabu inahitaji jambo moja tu..................................................................... 107

*Nikitaburuku kitabu hiki kwa waandishi wote wa Ki-Tanzania. Tusichoke kusoma na kuandika!*

# DIBAJI

**KILA WAKATI HUWA** namwambia Daudi, wewe siyo tu mwandishi bali ni mwalimu ambaye umeamua kujitolea kubeba maono na maumivu wanayopitia waandishi wa vitabu na kuja na mwarobaini. Na kwa hili la kuandika kitabu hiki cha Uandishi wa Vitabu Vinavyouzika, nampongeza.

Ngoja leo niseme hivi! Tasnia ya uandishi wa vitabu ni tamu sana na yenye mafanikio, tatizo kubwa waandishi wengi wanabahatisha, hawapendi kujifunza na hawalijui vizuri soko la vitabu. Hivyo uwepo wa

kitabu hiki mikononi mwako ni dalili njema ya kuelekea pazuri zaidi.

Kwa sababu kitabu hiki kimebeba ujumbe mzito na kimegusa taarifa zote muhimu unazohitaji kusikia ili kufikia kilele cha uandishi bora wa kitabu kinachouzika. Kimekidhi kiu na matakwa halisi ya soko la uandishi wa vitabu kwenye karne hii hatua kwa hatua na kwa vitendo. Siyo tu kuandika, bali na jinsi ya kukitoa kitabu chako na kuwafikia walengwa au soko lako.

Zaidi ya hayo, kitabu hiki kimeandikwa kwa lugha rahisi ambayo inaeleweka na kinafaa kusomwa na kufanyia kazi yale utajifunza ndani yake. Ni imani yangu wewe kama msomaji ama mwandishi utanufaika sana baada ya kusoma kitabu hiki kinachojibu maswali ya waandishi.

Huu ni ufunguo – *chukua!.*

**Raymond Medard**
**| Mwandishi | Copywriter**

# UTANGULIZI

**WATU WENGI WANAOTAMANI** kuandika, kutoa ama kuuza vitabu vyao huwa hawana mtu wa kuwashika mkono na kuwasaidia pale wanapokwama na mambo kwenda ndivyo sivyo.

Nije kwako!, sasa kitabu hiki kipo mikononi mwako na leo utaanza kusoma siku ya kwanza katika safari ya siku 25 zilizo mbele yako, lakini Je! Wewe umekwama katika changamoto ipi?. Nataka nikutoe wasiwasi kwamba mara unapoanza kukisoma nitakuwa nakupatia majibu ya mahali ulipokwama.

Nimekiandika kitabu hiki nikiwa na hamasa kubwa ya kuona wewe unasaidika, iwe upo kwenye hatua ya kuandika, kutoa au kuuza kitabu chako. Kuanzia siku ya 1 mpaka ya 25 nimekusanya mambo mbalimbali yanayogusa kila eneo la uandishi wa vitabu, na kama nilivyosema hapo awali, nitagusa na eneo lako unalotamani kujua.

Kitabu hiki si mwisho wa kukusaidia wewe. Natamani sana kwamba unapotaka usaidizi zaidi, usisite kuwasiliana nami na nitafurahi kukusaidia.

*Nisikuchoshe! Anza kusoma sasa!*

# Siku ya 1

## Tabia 5 zinazoleta mafanikio kwa mwandishi

KILA MWANDISHI WA vitabu hutaka kufanikiwa lakini mafanikio huchagizwa na tabia anazokuwa nazo mwandishi mwenyewe. Kuna tabia tano ambazo mwandishi akiwa nazo basi mafanikio huja yenyewe.

**1. Tabia ya kuandika kila siku.** Kuandika kila siku si jambo dogo na pengine unajiuliza, *"hili linawezekanaje?"*. Lakini unaweza kutenga dakika 5 mpaka 10 kila siku kwa ajili ya kuandika, hata

kama ni kitu kidogo kiandike. Unaweza kutenga dakika hizo mida ya asubuhi - mapema unapoamka, usiku kabla ya kulala au mchana baada ya kutoka lunch. Misuli yako kama mwandishi hupashwa kila siku unapoandika.

**2. Tabia ya kusoma kadri unavyoweza.** Huwa wanasema mwandishi mzuri ni msomaji mzuri. Soma vitabu vya waandishi mbalimbali, hata vile ambavyo sivyo vya aina unayoandika wewe. Unapofanya hivyo unapata ladha mbalimbali za waandishi wengine na itakufanya wewe kuwa bora zaidi

**3. Tabia ya kujiwekea malengo yaliyo wazi.** Utapimaje mafanikio yako kama huweki malengo? Weka malengo yaliyo wazi, yanayopimika. Ni kweli kwamba, unaweza kutimiza malengo unayojua, na ambayo unaweza kujikumbusha.

**4. Tabia ya kupenda kutumia teknolojia.** Mwandishi lazima ujenge tabia ya kwenda na teknolojia. Si muda wote utatumia *Microsoft*

*Word* kuandika kitabu, nenda *playstore* au *appstore* na pakua aplikesheni kama vile *evernote, zoho note, google writer* na n.k. Huwezi kutembea na kalenda kila mahali ili kujikumbusha malengo yako, jizoeze kutumia *google* kalenda. Ninachosema hapa ni kwamba, tumia teknolojia na zipo teknolojia nyingi mno, jizoeze kuzitumia.

**5. Tabia ya kumaliza kila unachoanza.** Uwe na tabia ya kumalizia vitabu unavyoandika, usiandike kitabu kipya halafu ukaishia njiani pasina kukimaliza. Najua ni ngumu, lakini inawezekana. Kumbuka nguvu uliyoweka ulipoanza kuandika, ukiishia njiani umepoteza muda na nguvu yote uliyoweka.

# Siku ya 2

## Fanyia kazi mambo haya manne (4) ufanikiwe zaidi.

**KWENYE TASNIA YA** uandishi wa vitabu hakuna msahafu mmoja wa kuufuata ili ufanikiwe kwenye uandishi. Kila siku kuna njia mpya na mambo mapya ya kufanya ili uandishi wako uwe na mafanikio. Mara nyingi mafanikio kwenye uandishi wa vitabu ni kuona matunda ya kazi yako na kuyafaidi.

Ni kweli, yapo mambo yasiyobadilika ili mwandishi awe na mafanikio, hayo ni mambo ya msingi kwenye uandishi wa vitabu. Tumekukusanyia mambo manne (4) ya kuongezea kwenye hayo unayoyajua tayari, huu ni kama ushauri wangu kwako uweze kufanikiwa zaidi. Mambo hayo ni haya,

1. **Andika kitabu kisichochosha.** Kama ukiwauliza wasomaji wa vitabu ni jambo gani huwafanya wasimalize kuvisoma baadhi ya vitabu fulani watakwambia vitabu ambavyo haviwapi hamasa na vinavyochosha.

   Kama mwandishi wa vitabu, ushauri wangu ni kuwa, kila unapoandika kitabu kipya, basi hakikisha kitabu chako kuanzia kurasa ya kwanza mpaka ya mwisho kinampa ladha tamu msomaji kiasi kwamba atakiweka kitabu chini akiwa amemaliza kukisoma. Hapa ndiyo kuna siri ya kutofautisha kitabu kinachouza na kile kisichouza. Fanyia kazi jambo hili na utaona mafanikio.

**2. Kuwa mkweli unapozungumzia kitabu chako**. Usiwe mmoja ya waandishi ambao anakipamba kitabu chake mno halafu msomaji akinunua anakuta hamna kitu, ni maneno matupu tu ya mwandishi. Kitabu chako kiwe na jalada *(kava)* bora ambalo litasadifu yaliyomo ndani ya kitabu. Usitie chumvi mno huku unajua kitabu chako ni cha kawaida sana. Ukifanya hivyo, utaathiri mauzo ya kitabu chako kinachofuata, wasomaji watajua ni zile porojo zako, kumbe sasa umetoa kitabu kizuri mno. Jambo la muhimu ni kuwa mkweli na ikiwezekana weka bei ya chini kama unajua kitabu si bora sana. Ukifanyia kazi hili lazima utafanikiwa.

**3. Zungumza na wasomaji wako.** Kuna waandishi ambao wasomaji wake wakitaka kusema naye jambo hawana namna ya kumfikia. Kama ni kwenye mitandao hajibu meseji za iniboksi, hajibu baruapepe na n.k. Siri ni hii, ukitaka kufanikiwa chukua ushauri huu,

zungumza na wasomaji wako, jichanganye kwenye mitandao hasa Facebook na utaona namna wasomaji wako wanakuwa karibu na wewe zaidi.

**4. Pata maoni ya wasomaji na yafanyie kazi.** Mara nyingi wasomaji hutoa maoni kwa mwandishi wanapomaliza kusoma vitabu vyao. Sasa ukipata yale maoni yafanyie kazi na wape mrejesho wasomaji wako. Ukifanyia kazi hili, mafanikio yanakuja tu yenyewe.

# Siku ya 3

## Unaupataje muda wa kuandika kitabu?

S**WALI GUMU AMBALO** kila mtu anayetaka kuandika kitabu hujiuliza ni, *"napataje muda wa kuandika kitabu?*", Majibu ya swali hili si magumu wala si mepesi kwa sababu kila mtu ana masaa yale yale 24 lakini kuna mwingine ataweza kuandika kitabu na mwingine atashindwa kuandika kitabu.

Tuna mambo mengi tunayofanya na yote yanataka nafasi ya kufanyika ndani ya haya masaa 24

tuliyonayo. Pengine nukuu ya Toni Morrison inayosema *"Write at the edges of the day."* Inaweza kutupa mwanga wa kuanzia kujibu swali hili la kuupata muda wa kuandika kitabu. Ki msingi anachosema Toni ni kuwa, unaweza pata muda wa kuandika kitabu chako mwanzoni mwa siku au mwishoni mwa siku.

## Mwanzoni au mwishoni kwa siku.

Kama wewe ni mtu wa kuamka mapema sana kujiandaa kwenda kwenye majukumu yako ya siku, basi muda wa asubuhi sana ndiyo unaweza kuutumia kuandika kitabu. Hii inawafaa sana watu walioajiriwa wanaotaka kuandika kitabu. Mwandishi wa vitabu Joanna Penn  amewahi kutumia mbinu hii, anasema kuwa *"Niliandika kitabu changu cha kwanza nilipokuwa mwajiriwa. Nilikuwa naamka saa kumi na moja alfajiri, na baada ya kujiandaa kwenda kazini, nilikaa kuandika kitabu kwanza kwa sababu kazini nilikosa muda na baada ya kutoka kazini nisingeweza kuandika kwa sababu ya uchovu".*

Si kila mtu ataweza kuandika asubuhi sana anapoamka, kuna wengine wataweza kuandika muda wa usiku baada ya kutoka kazini. Binafsi, nimeandika baadhi ya vitabu vyangu wakati wa usiku nikiwa nimetulia.

Kwa hiyo, siku inapoanza unaweza kuandika kitabu au siku yako inapoisha unaweza kuandika kitabu pia.

## Kitu gani unaweza kukiachilia au kukiacha ili upate muda wa kuandika?

Umeshindwa kupata muda asubuhi au usiku, nini ufanye sasa? Angalia katika vitu unavyofanya mchana, kipi ukiache ili utengeneze muda hapo wa kuandika kitabu. Mfano, kama unaangalia TV kwa masaa matatu, punguza muda hapa, angalia TV kwa lisaa limoja tu na masaa mawili yanayobakia yatoe kuandika kitabu.

Kama upo kazini, ule muda wa kupiga soga na wenzio wakati mmejipumzisha, wewe utumie kuandika kitabu.

## Vipi ule muda upo kwenye gari au daladala?

Muda mwingi unapotea tunapokuwa kwenye gari au daladala kwa sababu ya, mfano, foleni. Muda huu unaweza kuutumia kuandika kitabu pia. Kama upo kwenye foleni masaa mawili, fikiria ni kurasa ngapi utakuwa umeweza kuandika? Bila shaka nyingi sana.

## Jambo la muhimu ni nini?

Muda unatengenezwa! Jambo lolote ukitaka kulifanya lazima utalitengenezea muda wa kulifanya. Joann Penn anasema *"it's all about scheduling"*. Ni wewe tu kuweka ratiba na kuamua kuifuata. Pangilia muda wa kuandika kitabu na hakikisha unautumia kuandika.

*Umefurahia safari ya siku hizi 3? Bado siku 22 mbele yako, Je! ungependa kuendelea?*

*Bonyeza hapa chini*

**Nataka kuendelea >**

**Mara unapobonyeza, utakuja WhatsApp moja kwa moja*